LUKENYA UNIVERSITY

ISSN 2663-3183 MULTIDISCIPLINARY JOURNAL (LUMJ)

Vol 1, (1), p.78-84

Matumizi ya Mbinu ya Weusi na Uwili: Tathmini ya Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea

Dkt. Dorcas Muendi Musyimi

Chuo Kikuu cha Chuka

musyimidorcas@yahoo.com

https://orcid.org/0000-0001-9439-727X

Article history
Received: August 10, 2020
Received in revised form: September 21, 2020
Accepted: November 9, 2020
Available online: https://research.lukenyauniversity.ac.ke/

IKISIRI

Kulingana na Wamitila (2008), matumizi ya mtindo katika kazi za fasihi ndicho kipengele ambacho humtofautisha mtunzi mmoja na mwingine. Hii inatokana na ukweli kwamba kila mtunzi anao mtindo wake wa kuwasilisha jambo mbele ya hadhira yake kwa namna ambayo yeye binafsi anaona kuwa ni sahihi kufanya hivyo. Basi, lengo la makala haya ni kubainisha matumizi ya mbinu ya weusi na ya uwili katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora. Isitoshe, makala haya yataeleza dhima ya weusi na uwili katika riwaya hii. Makala haya yametumikiza nadharia ya Elimu-mtindo kwa mtazamo wa Leech na Short (1981). Data ya makala ilipatikana maktabani kwa kusoma riwaya teule kisha ikachanganuliwa kwa misingi ya nadharia iliyoteuliwa na lengo la makala. Ilibainika kuwa mwandishi ametumia mbinu ya weusi ili kuashiria kukosa tumaini, matatizo ya wahusika, dhuluma dhidi ya Waafrika kutoka kwa Wakoloni, hatari, kutoshughulikiwa, ukali, na pia tisho. Mtafiti alibaini kuwa sababu zilizomfanya mwandishi kutumia mbinu ya uwili ili kuashiria ubunifu na uhuru wake katika utunzi.

Istilahi Muhimu: Weusi, Uwili, Elimu-mtindo.

1.0 Utangulizi

Kulingana na Wamitila (2002), mtindo ni kipengele cha fani ambacho huelezwa na wataalamu wa fasihi kama namna au jinsi mtunzi wa kazi ya fasihi anavyoiunda kazi yake na kuiwasilisha kwa hadhira iliyokusudiwa kwa ujumbe na dhamira ile ile aliyotaka hadhira iipate. Naye Msokile (1993) katika kufafanua dhana ya mtindo, anaeleza kuwa mtindo unaweza ukabainishwa katika makundi matatu ambayo ni namna msanii anavyoyawasilisha mawazo yake kwa hadhira, namna ya uandishi kwa kipindi fulani cha kihistoria,

ufundi, umahiri na hisia za mtu binafsi katika kutenda kazi yake. Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa uhuru wa msanii kwa kawaida hubainika katika vipengele vya fani na maudhui ambavyo humpa upekee wake. Wachambuzi wengine wa kazi za sanaa huita mtindo. Ni kutokana na maelezo haya ambapo makala haya yalikusudia kubainisha sababu kuu za mwandishi za kutumia mbinu ya weusi na ya uwili katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*.

1.1. Wasifu wa Mwandishi Ken Walibora

Kulingana na Mbati (2020) na Cheruiyot (2020), Ken walibora alizaliwa Januari 6, mwaka 1964 kama mtoto wa tatu (kitinda mimba) wa Peter Wafula na Ruth Nasambu Makali na kuitwa jina la Kennedy Walibora Waliaula huko Baraki, kaunti ya Bungoma magharibi mwa Kenya, kisha wakahamia Kitale akiwa na miaka minne na baadaye Cherangany. Mamake aliaga 1984 akiwa miaka 51 kutokana na ugonjwa wa muda mrefu. Ken alikuwa na umri wa miaka 20. Naye babake aliaga mwaka wa 2006. Mwandishi alikuwa na majina mawili ya Kiingereza, Kenny na George. Alichagua kutumia jina Kennedy. Baadaye alibadili jina lake na kufahamika kama Walibora, ambalo lilikuwa linamaanisha kuwa ni bora kwa Kiswahili na kufupisha jina lake la kwanza kuwa Ken. Baada ya mamake kuaga, Ken alilelewa na mamake wa kambo Eunice Wafula.

Kulingana na tawasifu ya Ken Walibora katika riwaya ya *Nasikia Sauti ya Mama* (Walibora 2014) walihama Baraki baada ya kifo cha ndugu yake ambaye inaaminika alitiliwa sumu na mke wa ndugu wa kambo wa babake. Baada ya kakaye Ken kufa na kuzikwa yule muuaji alipania kumuua Ken Walibora ambaye alikuwa bado hajafikisha mwaka mmoja. Mtuhumiwa anakisiwa kuwa alienda akamchukua Ken kutoka kwa dadake ambaye alikuwa amempakata, akaenda naye nyuma ya nyumba kisha dadake kumfuata ndiposa akashuhudia akimlisha kitu cha ajabu. Baada ya hapo afya Ken ilidhoofika lakini kwa bahati nzuri akaokolewa na wataalamu wa kuganga matatizo ya aina hiyo.

Alipofikisha umri wa kwenda shule mwaka wa 1971 alijiunga na shule zifuatazo: Shule ya msingi ya St. Joseph- Teremi, Shule ya upili ya Suremi, shule ya upili ya Ole Kajiado, Chuo Kikuu cha Nairobi na chuo kikuu cha Ohio-Marekani. Aliaga dunia baada ya kugongwa na gari tarehe 10 Aprili 2020. Ken Walibora aliandika vitabu kama vile *Siku Njema* (1996), *Ndoto ya Amerika* (2001), *Kufa Kuzikana (*2003), *Kidagaa Kimemwozea* (2012), *Ndoto ya Almasi* (2012) na *Nasikia Sauti ya Mama* (2014). Alishirikiana na Said Mohamed katika kuandika kitabu cha hadithi fupi cha *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2013).

Gikambi (2020), anasema kuwa Ken alifariki tarehe 10 Aprili 2020 baada ya kugongwa na gari, Nairobi kama polisi walivyoripoti. Alizikwa Jumatano tarehe 22 Aprili 2020 nyumbani kwake Makutano kwa Ngozi, jimbo la Cherang'any huko kaunti ya Trans Nzoia magharibi mwa Kenya.

1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea.*

Riwaya hii inawahusu wahusika wawili Amani na Imani ambao wako safarini kwenda Sokomoko ili kusaka ukweli kuhusu changamoto za familia zao. Wanapata ajira kwa Mtemi Nasaba Bora na Majisifu mtawalia. Hatima ya safari yao ni kuwa wanapata hatimiliki za ardhi za wazazi wao zilizokuwa zimechukuliwa na Mtemi Nasaba Bora. Amani aliamua kuwagawia vijisehemu baadhi ya wahusika waliokuwa wamepokonywa ardhi na waliokuwa bila kama Matuko Weye. Amani alishirikiana na

Madhubuti, mtoto wa Nasaba Bora ili kuunda jamii mpya ya Wanasokomoko.

2.0 Nadharia ya Utafiti

Makala haya yametumikiza nadharia ya Elimu-Mtindo. Fasili ya mtindo bado ina utata kwa maana ziko namna tofauti za kuifasili dhana hii ya mtindo. Ila kwa mtazamo wa hivi karibuni yaani karne ya 20, wataalamu kama Leech na Short (1981), Halliday na Hassan (1971) na Enkvist (1973) wanauona mtindo kuwa ni uchaguzi au ni utofauti. Elimumtindo ni nadharia ambayo hutumia njia na utafiti wa sayansi ya lugha kuchambua kazi za fasihi. Nadharia hii ilianzishwa katika karne ya ishirini kwa lengo la kuonyesha namna mbinu za lugha zinavyotumiwa katika kazi za fasihi na athari yake katika maana ya kazi hizo. Mtindo pia huimarisha uwezo wetu wa kufikiri kuhusu lugha katika kuangalia uelewa wetu kuhusiana na kazi za fasihi. Hivyo elimu-mtindo inahusiana na namna ambavyo maneno hupangiliwa ili kuelezea ubinafsi wa mzungumzaji au mwandishi katika kutoa hisia au mawazo yake. Pia inajishughulisha na matumizi ya lugha katika mawasiliano, yaani ubunifu katika utendaji kazi wa lugha. Kila mwandishi ana namna ya pekee katika kutoa mawazo yake tofauti na waandishi wengine. Kwa kutumia msingi wa elimu-mtindo ambao ni ubunifu katika nyanja za lugha, makala haya yalichunguza namna mwandishi alivyotumia mbinu ya weusi na uwili katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*.

2.1 Mtindo kama Utofauti

Kulingana na Enkvist (keshatajwa), mtindo ni kama kanuni za utofauti katika kazi ya mwandishi. Kazi mbalimbali za kisanii huwa na utofauti hususan riwaya, tamthilia na ushairi. Kwa ujumla, mtindo unaweza kutafsiriwa kuwa namna lugha inavyoweza kutumika kiutofauti kutegemea hadhira, muktadha na lengo.

Mtindo hujumlisha lugha ya mazungumzo pamoja na ya maandishi. Aidha, unahusu kazi za kisanii zilizoandikwa na zile ambazo si za kisanii. Ni kutokana na haya ambapo Leech na Short (keshatajwa), wanadai kuwa:

> "Katika uwanja wa uandishi, kuna fasili mbalimbali kama vile upekee wa mwandishi kwa namna alivyoamua kuitumia lugha. Kwa upande mwingine, ni jinsi lugha inavyotumika kulingana na aina ya kazi, kipindi au kiwakati ilipotungwa, shule ya kitaaluma na mjumuiko wa yote kwa pamoja" (1981).

Maelezo haya yanaashiria kuwa kwa sababu lugha ina sifa ya kuweza kunyambulika, msemaji au mwandishi ana uwezo wa kuinyambua lugha kwa namna yake mwenyewe na hatimaye kuwa mazoea. Mazoea hayo huweza kufungamanisha naye katika mpito wa wakati. Kutokana na kule kutumia vipengele mbalimbali vya lugha, hivyo ndivyo hutumiwa ili kuonyesha mtindo wa msemaji au mwandishi.

3.0 Mbinu za Utafiti

Data ya makala haya ilipatikana kwa kuipitia riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora, 2012) na kisha kuichanganua kwa kudondoa mbinu za uandishi za weusi na uwili kulingana na lengo la makala.

4.0. Matumizi ya mbinu ya Weusi na ya Uwili katika *Kidagaa Kimemwozea*

Baada ya kuipitia riwaya teule, mtafiti amegundua kuwa kunao matumizi ya mbinu ya weusi na ya uwili.

4.1 Mbinu ya Weusi.

Ndonye (2017), anasema kuwa rangi mbali mbali katika kazi za kifasihi hutumiwa kuashiria mambo mbalimbali ambayo yana uhalisia katika maisha ya banadamu. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya

TATAKI (2014), weusi ni rangi yenye giza kama vile ya makaa au lami. Rangi hii huweza kuashiria giza au majuto. Aidha, rangi nyeusi inaweza kuashiria matatizo au shida, mauti au kifo, uovu au hatari fulani na hata siri. Siri ni mambo yasiyotamanika kujulikana kwa watu au kwa wale wasiohusika kwayo. Isitoshe, rangi nyeusi huashiria kutokuwa na matumaini na hata kuwa katika hali ya taharuki.

Ifahamike kuwa, kila mwandishi anapoandika kazi yake hukusudia kuwasilisha jambo jipya katika ulimwengu wa utunzi (Ndonye, 2017). Kutokana na maelezo haya, mtafiti anakusudia kubainisha lengo la mwandishi la kutumia weusi katika uandishi wake.

Katika uk 1, mwandishi anaeleza kuwa Amani alikuwa na mkoba mdogo mweusi uliobeba kila kilichokuwa chake. Hii ina maana kwamba mhusika huyu alikuwa kijana asiye na tumaini kwani alikuwa ametoka kwao Ulitima (kumaanisha umaskini) akiwa amevaa sharti lililodondosha vifungo. Suruali yake ilikuwa na viraka viwili vikubwa vilivyochungulia makalioni kama vazia.

Katika safari yake ya kwenda Sokomoko, Amani alipatana na msichana Imani aliyekuwa na ngozi iliyokoza weusi kiasi cha watu kumwita "cheusi dawa" (uk 1) Mwandishi ameitumia rangi hii kwa nia ya kuonyesha machungu aliyokuwa nayo Imani baada ya watu wasiojulikana kuchoma nyumba yao na kumpiga mamake.

Kijana DJ alipokuwa akiogelea bila kujali, fahali mmoja mkubwa mweusi aliyekuwa analishwa karibu na kaptula moja kuukuu, aliizoa kinywani na kuanza kuisagasaga (uk 7). DJ alibaki bila nguo. Machozi yalimtoka njia mbili mbili tu ishara ya kukosa tumaini. Ilimbidi Amani kumpa lake ili kujisetiri.

Kulingana na mwandishi, eneo la Sokomoko lilikuwa limetengewa Wazungu peke yao katika enzi ya ukoloni (uk 12). Watu weusi nao walitengewa sehemu kama vile Ulitima na Mabondeni. Hata hawakuruhusiwa kumiliki walau ndama wala mwembe mmoja huko Sokomoko. Watu weusi walitakiwa kufuga mifugo ya kienyeji na iwe ni nje ya Sokomoko. Aidha, ilikuwa ni haramu kwao kupanda mazao yaletayo faida. Rangi nyeusi kwa Mwafrika iliashiria unyanyasaji kutoka kwa wakoloni kwa sababu ya rangi yake. Waafrika walidhulumiwa kwa njia zozote zile.

Katika maskani ya Mtemi Nasaba Bora, kulikuwa na majibwa mawili meusi ambayo yaliwabwekea Amani na Imani (uk 20). Mtemi aliwatumia ili kuwatia hofu wote waliomtembelea. Mwandishi anasema kwamba jibwa moja liitwalo Jimmy liliishia kumng'ata DJ. Lilikuwa likiugua ugonjwa wa *rabbies* (uk 104).

Mtemi Nasaba Bora alimiliki gari la aina ya *Nissan Sunny*. Amani na Imani walipomtembelea walimsaidia kulisukuma huku likitoa wingu kubwa la moshi mweusi (uk 22). Kitambo likiwa nzuri lakini Mtemi mwenyewe hakutaka kutumia hela nyingi kulifanyia matengenezo yahitajikayo au kununua jipya. Moshi huu mweusi ulikuwa na ishara ya gari hili kutoshughulikiwa basi kuwa na matatizo anuwai.

Katika ukurasa wa 36, mwandishi anaelezea jinsi Amani alivyokipata kitoto cheusi kivulana chenye siha nzuri na miguu ya matege kimeachwa mlangoni mwa kibanda chake. Hakujua asili wala fasili yacho. Weusi huu ulikuwa na ishara ya kukosa matumaini kwani kilikuwa kimekataliwa na wazazi wake waliokuwa Mtemi Nasaba Bora na Lowela, msichana wa Maozi aliyekuwa mwajiri wa DJ. Hatimaye, kitoto hiki kilikufa

kutokana na ugonjwa wa homa ya matumbo (uk 77).

Amani anaeleza kuwa baada ya kutoka kifungoni alipokuwa amefungwa kwa masingizio ya wanafunzi wenzake, alitembelea familia ya Fao waliyesoma naye na kukutana na dadake Fao, msichana mnene mweusi aliyekuwa kazaa mtoto ingawa alikuwa hajaolewa hata chuo kimoja (uk 36). Msichana huyu alikuwa kakosa tumaini katika maisha.

Baada ya kitoto Uhuru kufa, Amani na Imani watiwa ndani na Mtemi Nasaba Bora kwa tuhuma za kumuua. Walipotiwa seli walipatana na askari mmoja mrefu kama twiga na mweusi kama usiku ambaye aliukomolea mlango kwa nguvu (uk 83). Nia yake ilikuwa ni kuwatia hofu na kuwaonyesha kuwa hawakuwa na matumaini ya kutoka pale. Alitumiwa kuwatisha kwa kuwaita wauaji waliostahili kifo kama kitoto Uhuru.

Mzee Matuko Weye alimwambia Imani walipokutana seli kuwa mkoloni Mzungu alikuwa afadhali kuliko mkoloni mweusi (uk 85). Mhusika huyu alikuwa ameshuhudia unyanyasaji wa watu weusi kutoka kwa wenzao weusi kama Mtemi Nasaba Bora ambaye alikuwa ameyanyakua mashamba ya raia wa Sokomoko kama lile la kina Imani na kumuua babuye Amani aliyeitwa Hamadi Chichiri. Aidha, Mtemi alikuwa amemchumbia Lowela, msichana mdogo wa Maozi. Raia walikuwa wamekosa tumaini chini ya utawala wa viongozi weusi.

Mtemi Nasaba Bora aliwatembelea Amani na Imani katika seli na gari lake lilipoondoka, mwandishi anasema kwamba liliacha nyuma wingu kubwa la moshi mweusi (uk 89). Mara tu alipoondoka mahabusu Imani na Amani walianza kufanyiwa kazi. Askari waliwapiga bila huruma. Moshi huo uliashiria ukatili waliokabiliana nao Imani na Amani katika mikono ya askari.

Kwa jumla, mwandishi ametumia mbinu ya weusi ili kuashiria taharuki, kutoshughulikiwa, kukosa matumaini, hofu, matatizo, ukatili, giza na hatari.

4.2 Mbinu ya Uwili

Mwandishi anaonekana kupanga wahusika wake katika jozi. Katika kuzungumzia suala hili, Wamitila (2003) anasema kwamba, dhana ya mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Aidha, ni jinsi mwandishi fulani anavyojieleza katika kazi yake. Kila msanii hujitahidi kubuni ili kujitofautisha na wasanii wengine.

Katika ukurasa 1, kunao vijana wawili Amani na Imani ambao wako safarini kwenda Sokomoko ambako wanapata ajira kwa Mtemi Nasaba Bora na nduguye Majisifu mtawalia. Mwandishi amewatumia wahusika hawa wanne kama wahusika wakuu katika riwaya husika.

Riwaya hii inahusu hadithi mbili. Mojawapo ni hadithi kuu *Kidagaa Kimemwozea* na kuna mswada wa *Kidagaa Kimemwozea* ambao unasemekana kuibiwa na Majisifu ukiwa umeandikwa na Amani. Riwaya ya pili inaibua mgogoro wa wizi wa miswada huku ikitumika kama hadithi ndani ya hadithi. Hadithi kuu nayo inaangazia kuharibikiwa kwa mambo kwa wahusika wake.

DJ alipokutana na Imani na Amani kando ya Mto Kiberenge (uk 3), kando ya kichaka kulikuwapo na tumbili wawili, mmoja jike na mwingine dume. Mwandishi anaeleza kuwa wakazi wa karibu na Mto Kiberenge, wa ng'ambo zote mbili walitunga wimbo uliotangaza mwiko wao wa kutoyanywa maji yake. DJ na wenzake walishangaa walipowaona Amani na Imani wakivunja mwiko huo kwa kuyanywa maji yale.

Baada ya ng'ombe kusagasaga nguo ya DJ, machozi yalimtoka njia mbili mbili (uk 8). Kijana huyu hakuwa na nguo nyingine. Ilimbidi Amani kumpa nguo yake ili kujisetiri. Miaka miwili baada ya DJ kukutana na Amani na Imani, mguu wake wa kushoto ulikuja kung'atwa na mbwa. DJ alilazwa hospitalini. Amani na Imani walipoenda kumtembelea walimkosa. Walidhania kuwa katoroka. Kumbe, alikuwa ametoroka kwenda kutafuta matibabu kwa waganga wa dawa za kienyeji. Hatimaye, alipona na kukutana na Amani na Imani.

Mbinu ya uwili imetumika pia katika kuashiria watoto wawili wa Mtemi Nasaba Bora; Madhubuti na Mashaka. Aidha, Majisifu alikuwa na mapacha wawili huku mhusika Maozi akiwa na watoto Lowela na Ben Bella. Mwandishi anaeleza kuwa Imani alikuwa na kakake wawili; Oscar Kambona na Chwechwe Makwechwe ilhali kuna wahusika wawili waliosomea ughaibuni; Fao na mtotoe Mtemi ambaye ni Madhubuti. Mwandishi amewasawiri wahusika walio wawili wawili ili kuonyesha ubunifu na ustadi wake katika kuandika kazi yake.

Kabla ya Amani na Imani kufungwa jela bila hatia, mwandishi anasema kuwa walikuwa wamefanya kazi kwa waajiri wao Majisifu na Mtemi Nasaba Bora kwa miaka miwili miwili. Wahusika hawa walikuwa wamefungwa kwa kisingizio cha kukiua kitoto kilichokuwa kimeachwa nje ya kibanda cha Amani. Kitoto hiki kilikuwa cha Lowela na Mtemi ila kiliachwa nje ya kibanda kisicho cha wazazi wake. Mwandishi anaeleza kuwa, baada ya Fao kumringa msichana wa shule alikataa kumuoa. Alipoondoka kwenda kusomea ng'ambo, kitoto kile kililetwa nje ya nyumba ya wazazi wake na kuachwa pale.

Kinachodhihirika ni kwamba mwandishi ametumia mbinu ya uwili ili kuonyesha ubunifu wake. Hii ni ishara kuwa kila mwandishi ana namna ya pekee katika kutoa mawazo yake tofauti na waandishi wengine.

5.0 Hitimisho

Makala haya yamebainisha kuwa katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kuna matumizi ya mbinu za uandishi za weusi na uwili. Kila msanii hujitahidi kubuni ili kujitofautisha na wasanii wengine. Ubunifu katika kazi za sanaa husababishwa na athari alizozipata msanii kutokana na elimu aliyonayo, mazingira alimo au aliyokulia. Mwandishi ametumia mbinu ya weusi ili kuangazia kukosa tumaini, matatizo ya wahusika, dhuluma dhidi ya Waafrika, hatari, kutoshughulikiwa na pia tisho. Mtafiti alibaini kuwa sababu zilizomfanya mwandishi kutumia mbinu ya uwili ni kuashiria ubunifu na uhuru wake katika utunzi.

MAREJELEO

Cheruiyot, K. (2020). Ken Walibora: Life and times of renowned author. https://www.the-star.co.ke/news/2020-04-15-ken-walibora-life-and-times-of-renowned- Ilichukuliwa 22/8/2020.

Enskvist, N. E**. (**1973)**,** *Linguistic Stylistics*. Netherlands: Mouton (The Hague). https://www.abebooks.co.uk/book-search/title/linguistic stylistics/author/enkvist-nils-erik/ Ilichukuliwa 22/8/2020.

Gikambi, H. (2020), Ken walibora: Jinsi mfalme wa Kiswahili Kenya alivyonipatia msukumo maishani. https://www.bbc.com/swahili/habari-52451539 .Ilichukuliwa 24/8/2020.

Halliday, M. A. K. & Hasan R. (1991) *Language, context, and text: Aspects of Language in a Social-Semiotic Perspective*. Oxford University Press.

https://pdfs.semanticscholar.org/dbe8/fe03455c40d77538f473c08da215a2103496.pdf?_ga=2.137661168.1102545785.1598020199-508375134.1598020199 Ilichukuliwa 23/8/2020.

Leech, G. N., & Short, M. H. (1981). *Style in Fiction*. London: Longman.

https://www.scirp.org/reference/ReferencesPapers.aspx?ReferenceID=1365711 Ilichukuliwa 22/8/2020.

Mbati, J. (2020). Veteran Author Ken Walibora Found Dead. https://www.kenyans.co.ke/news/52082-veteran-author-ken-walibora-dies. Ilichukuliwa 27/8/2020.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndonye, L. N. (2017). Rangi kama Mbinu ya Usimbaji maana katika Diwani ya Rangi ya Anga (Kithaka Wa Mberia). Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. http://erepository.uonbi.ac.ke:8080/bitstream/handle/11295/101918/Ndonye_Rangi%20Kama%20Mbinu%20Ya%20Usimbaji%20Maana%20Katika%20Diwani%20Ya%20Rangi%20Ya%20Anga%20%28Kithaka%20Wa%20Mberia%29.pdf?sequence=1&isAllowed=y. Ilichukuliwa 22/8/2020.

TATAKI. (2014), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la 3.* Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

_____(2003) Kichocheo cha Fasihi simulizi na Andishi. Nairobi: Focus Publication.

_____(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publications Limited.

_____ (2014). *Nasikia Sauti ya Mama*. Nairobi: Sasa Sema Publishers.